TANGAZO LA SERIKALI Na. 1105 la tarehe 27/12/2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA KILWA YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka, 2024.

Matumizi

**2.** Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Tafsiri

**3.** Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa au afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"shughuli za utamaduni" maana yake ni sanaa za maonyesho, sanaa za ufundi, muziki wa asili, michezo, muziki wa dansi, video, muziki wa taarabu, maonyesho ya sinema, mazingira, mazingaombwe, tiba za jadi na matumizi ya viwanja vya michezo;

"ushuru" maana yake ni malipo yatakayolipwa kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na Sheria Ndogo hii kutokana na huduma au bidhaaa

itakayouzwa, kununuliwa au kuingizwa na mtu yeyote ndani ya Halmashauri;

"usafiri kwa njia ya mtandao" maana yake ni huduma za usafirishaji zinazotolewa na vyombo vya usafiri kupitia mawasiliano ya mitandao ndani ya Halmashauri;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, Taasisi, Kampuni au Asasi yoyote iliyoteuliwa kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

Ushuru wa Huduma

**4.** Halmashauri itatoza ada au ushuru katika biashara, huduma, vibali, au leseni mbalimbali zinazotolewa ndani ya Halmashauri kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Huduma zitakazotozwa ada na ushuru

**5**. Halmashauri itatoza ada na ushuru katika huduma zifuatazo:

(a) ukodishaji wa mali za Halmashauri;

(b) ushuru wa kuvumisha matangazo (promotion);

(c) ushuru wa ukaguzi wa mifugo;

(d) ushuru wa vyoo vya umma;

(e) ushuru wa viwanda vya matofali;

(f) ushuru wa mazao ya bahari yanayouzwa katika mnada;

(g) ushuru wa kusafirisha samaki na mazao mengine ya bahari;

(h) ada ya maombi ya kujenga vituo vya kuoshea magari;

(i) ada ya ukaguzi wa afya kwa majengo mapya ya biashara;

(j) ada ya maombi ya zabuni mbalimbali za Halmashauri;

(k) ada ya kuweka majenereta;

(l) ada ya upimaji wa ubora wa maji ya visima, usajili wa jumuiya za watumia maji, ukaguzi, usimamizi na ufuatiliaji wa jumuiya za watumia maji na maombi ya kibali cha kutoa huduma ya maji;

(m) ada ya kuweka kontena la biashara kwenye eneo la Halmashauri;
(n) ada ya usajili na ushuru wa kuegesha vyombo vya uvuvi;
(o) ada ya matumizi ya fukwe za bahari;
(p) ushuru wa mgahawa wazi;
(q) ada ya kibali cha kituo cha kulaza magari kwenye maeneo binafsi;
(r) ada ya kupatiwa muhtasari wa Halmashauri;
(s) ada ya kibali cha kuendesha shughuli za gereji katika maeneo binafsi;
(t) ada ya kibali cha kufanya shughuli nyinginezo katika maeneo ya Halmashauri.

Namna ya kukusanya Ada na Ushuru

**6**.-(1) Halmashauri itaweka utaratibu kama itakavyoona inafaa ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo maalum ya kutoza ada na ushuru kutoka katika huduma mbalimbali zitakazoamriwa kutozwa ada au ushuru kama ilivyoainishwa kwenye kanuni ya 5.

(2) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au wakala na kutolewa stakabadhi halali ya kielektroniki kama uthibitisho wa malipo yaliofanyika.

(3) Endapo stakabadhi ya kieletroniki haiwezi kutolewa, Halmashauri au Wakala kwa idhini ya Mkurugenzi, itatoa kwa mlipaji stakabadhi halali ya kawaida kama uthibitisho wa malipo yaliyofanyika.

(4) Ada au ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kabla ya kupata huduma, leseni au kibali husika au baada ya kuuzwa au kununuliwa kwa bidhaa husika.

Ukamataji wa mali au mtu aliyekwepa kulipa ushuru.

**7**.-(1) Halmashauri au Wakala atakuwa na mamlaka ya kukamata bidhaa au mali ya mtu yeyote endapo ameshindwa kulipa ada au ushuru ndani ya muda aliotakiwa kulipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Endapo bidhaa au mali iliyokamatwa na Halmashauri au wakala haitalipiwa ada au ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa

zisizoharibika haraka, na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo baada ya kupata idhini ya mahakama kuuza bidhaa au mali hiyo na kukata fedha inayodai na kiasi kinachobakia atarudishiwa mmiliki.

(3) Wakala hataruhusiwa kuuza au kufanya jambo lolote kwa mali au bidhaa iliyokamatwa bila kupata idhini ya Mkurugenzi.

(4) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya Sheria Ndogo hii isipokuwa tu kama ikithibitika kuwa uharibifu huo umesababishwa na Halmashauri au Wakala wake.

(5) Halmashauri itatenga maeneo maalumu kwa ajili na kuweka mageti au vizuzi vya aina mbalimbali kwa lengo la kufanya ukaguzi wa ulipaji wa ushuru na ada kwenye huduma zitakazotakiwa kutozwa ada na ushuru.

Wajibu wa kusimama katika geti au kizuizi

**8**. Itakuwa ni wajibu kwa mtu yeyote anayetumia chombo cha usafiri kwa ajili ya kusafirisha bidhaa yoyote kusimama katika geti au kizuizi kilichowekwa na Halmashauri kwa ajili ya ukaguzi.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

**9**.-(1) Itakuwa ni wajibu kwa kila mtu anayetakiwa kulipa ada au ushuru, kulipa kiwango kama kilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hii

(2) Ni wajibu kwa kila mtu kutoa taarifa sahihi kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma, bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa ada au ushuru

(3) Itakuwa ni wajibu kwa kila mtu atakayelipa ada au ushuru kutunza kumbukumbu za malipo.

Kibali au leseni

**10.-**(1) Halmashauri itatoa kibali au leseni kwa mtu yeyote atakayewasilisha maombi ya kibali au leseni kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Itakuwa ni wajibu kwa kila mfanyabiashara anayetaka kufanya jambo lolote linalohitaji kibali au leseni kuomba na kupata leseni au kibali kutoka Halmashauri.

(3) Leseni yoyote itakayotolewa chini ya Sheria Ndogo hii itadumu kwa muda wa mwaka mmoja tangu tarehe ya kutolewa kwake.

(4) Itakuwa ni wajibu kwa wamiliki wa magari yafanyayo biashara ya usafirishaji kwa njia ya mtandao kuhakikisha wanakuwa na vibali vinavyowaruhusu kufanya biashara hiyo kwenye eneo la Halmashauri.

Usimamizi wa Sheria Ndogo hii

**11**.-(1) Halmashauri inaweza kusimamisha uendeshaji wa biashara au shughuli yoyote ambayo itafanyika bila laseni au kibali kilichotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ya 9(1), Halmashauri au Wakala wake wanaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa masharti ya sheria Ndogo hii.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kanuni ya 9(2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba, Halmashauri itauza kwa mnada bidhaa hizo baada ya kupata idhini ya mahakama na kutoa taarifa kwa mmiliki na umma kuhusu kusudio hilo.

Uteuzi wa Wakala

**12**. Halmashauri inaweza kumteua Wakala kwa ajili ya kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa Wakala

**13** Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hii atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hii.

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Makosa kwa Wakala

**14.** Itakuwa ni kosa kwa Wakala endapo-

(a) atajaribu au atakusanya ada au ushuru bila idhini ya Halmashauri;
(b) atajaribu au atakusanya ada au ushuru kwa kiwango tofauti kilichoidhinishwa kwenye Sheria Ndogo hii;
(c) atashindwa kuwasilisha au atawasilisha kiwango pungufu cha ada au ushuru kilichokubaliwa katika kukusanya ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii; au
(d) atashindwa kutoa stakabadhi halali ya malipo kwa ada au ushuru uliokusanywa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Uwezo wa Afisa Mwidhiniwa

**15**. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii; Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote au jengo lolote ndani ya muda wa kazi kwa nia ya kukusanya au kufanya tathimini au kufanya jambo lolote linalohusiana na ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa

**16**.-(1) Mtu yeyote anatenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii endapo:

(a) atashindwa, atadharau, atakwepa au atakataa kulipa ada au ushuru au atashindwa kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa ada au ushuru;
(c) atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri;
(e) atashindwa kutoa taarifa sahihi au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu huduma, bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa ada au ushuru; au

(f) atashindwa kutunza kumbukumbu sahihi za malipo ya ada au ushuru.

Adhabu

**17.** Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kutenda kosa chini ya Shrria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote.

Kufifilisha Kosa

**18.** Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa
TS Na.
22 la 2016

**19.** Sheria ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka 2016 inafutwa.

*Tangazo la serikali Na. 1105(linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4)*

SEHEMU YA KWANZA
UKODISHAJI WA MALI ZA HALMASHAURI

| Na. | Aina ya tozo | kiasi cha tozo |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba za Halmashauri | Kwa mujibu wa mkataba |
| 2. | Magari ya Halmashauri | Kwa mujibu wa mkataba |
| 3. | Ukumbi wa Halmashauri | Tsh. 200,000/= kwa siku |
| 4 | Viwanja vya wazi vya Halmashauri | 300,000/= kwa siku |
| 5 | Mitambo na Vifaa | Kwa mujibu wa mkataba |

SEHEMU YA PILI
USHURU WA MATANGAZO (PROMOTION)

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Biashara za Matangazo (promotion) kwa siku (binafsi) | Tsh 2,000 |
| 2. | Biashara za Matangazo (promotion) kwa siku (makampuni) | Tsh 5,000 |

SEHEMU YA TATU
UKAGUZI WA MIFUGO

A. Ada za Ukaguzi wa Mifugo

| Na. | Aina ya Mnyama | Machinjio ya Kawaida | | Machinjio ya Kisasa | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kabla ya Kuchinjwa Tsh | Baada ya Kuchinjwa Tsh | Kabla ya Kuchinjwa Tsh | Baada ya Kuchinjwa Tsh |
| 1. | Ng'ombe | 2,000/= | 2,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 2. | Mbuzi/Kondoo | 1,000/= | 1,000/= | 5,000/= | 5,000/= |
| 3. | Nguruwe | 5,000/= | 5000/= | 5,000/= | 5,000= |
| 4. | Kuku | 500/= | 500/= | 1,000/= | 1,000/= |

B. Ada za leseni za Eneo, Uchunaji wa ngozi na Upangaji wa madaraja

| Na. | Ada za leseni za Eneo | Kiwango |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya leseni uchunaji | Tshs 10,000/= kwa miaka mitatu |
| 2. | Ada ya maombi ya leseni ya uchunaji | Tsh. 5000 kwa kila ombi |
| 3. | Ada ya leseni ya upangaji madaraja | Tsh.10,000 kwa muda wa miaka mitatu |
| 4. | Ada ya maombi ya leseni ya kupanga madaraja | Tsh.5000 kwa kila ombi |
| 5. | Ada ya Leseni ya banda la kukaushia ngozi | Tshs 100,000/= kwa mwaka |
| 6. | Ada ya fomu ya maombi ya leseni ya banda la kukaushia ngozi | Tsh.20,000 kwa ombi |

*Tangazo la serikali Na. 1105(linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Ada ya Stika ya gari la kubebea ngozi kwa mwaka | Tsh.15,000/= kwa ombi |
| 8. | Ukaguzi wa afya kwa mwaka | Tsh.40,000/= |
| 9. | Usajili wa vikundi vinavyojishughulisha na zao la ngozi kwa mwaka | Tsh. 100,000/= |
| 10. | Leseni ghala la kuhifadhia ngozi zaidi ya 500 kwa mwaka | Tsh.100,000/= |
| 11. | Leseni ghala la kuhifadhia ngozi 100 - 500 kwa mwaka | Tsh.50,000/= |
| 12. | Leseni ghala la kuhifadhia ngozi chini ya 100 kwa mwaka | Tsh.10,000/= |
| 13. | a. Kuuza ngozi mbichi Machinjio (Wakusanyaji) kwa kipande | Tsh.100/= |
| | b. Kuuza ngozi zenye chumvi (wasindikaji) kwa kipande | Tsh.200/= |
| 14. | a. Kibali cha kusafirisha ngozi zilizosindikwa zaidi ya tani 5 kwa safari | Tsh 150,000/= |
| | b. Kibali cha kusafirisha ngozi zilizosindikwa, tani 1 hadi tani 5 kwa safari | Tsh 100,000/= |
| | c. Kibali cha kusafirisha ngozi zilizosindikwa chini ya tani 1 kwa safari | Tsh 25,000/= |

C. Ada Nyinginezo za Huduma ya Mifugo

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi Tsh. |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya kutunza Ng'ombe mmoja machinjioni kwa siku | 30,000/= |
| 2 | Ada ya kutunza Mbuzi/Kondoo mmoja machinjioni kwa siku | 10,000/= |
| 3 | Ada ya kusafirisha nyama kwa gari chini ya tani moja kwa safari | 5,000/= |
| 4 | Ada ya kusafirisha nyama kwa gari ya tani 1 hadi 5 kwa safari | 5,000/= |
| 5 | Ada ya kusafirisha nyama kwa gari ya zaidi ya tani 5 kwa safari | 10,000/= |
| 6 | Ada ya huduma ya ndani Kliniki ya mifugo | 5,000/= |
| 7 | Ada ya huduma ya nje ya Kliniki ya mifugo | 10,000/= |
| 8 | Ada ya uhamilishaji kwa ng'ombe mmoja | 5,000/= |
| 9 | Ada ya chanjo za mifugo | Kulingana na bei ya soko na miongozo itakayotolewa na Serikali. |
| 10 | Ada ya machinjio kwa ng'ombe | 2000/= |
| 11 | Ada ya machinjio kwa mbuzi/kondoo | 500/= |
| 12 | Ada ya kuchinja ng'ombe | 15,000/= |
| 13 | Ada ya kuchinja mbuzi/kondoo | 2000/= |
| 14 | Kibebeo cha nyama ya ng'ombe kwa safari | 1000/= |

*Tangazo la serikali Na. 1105(linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 15 | Kibebeo cha nyama ya mbuzi/kondoo | 1000/= |
| 16 | Ada ya soko/mnada wa wanyama wakubwa kwa mnyama | 5000/= |
| 17 | Ada ya soko/mnada wa wanyama wadogo kwa mnyama | 2000/= |
| 18 | Ada ya kukagua mifugo inayosafirishwa | 10,000/= |
| 19 | Ada ya kuchinja nguruwe mmoja | 2,000/= |
| 20 | Ada ya machinjio ya nguruwe kwa nguruwe mmoja | 2,000/= |
| 21 | Ada ya machinjio ya kuku kwa kuku mmoja | 100/= |

SEHEMU YA NNE
USHURU WA VYOO VYA UMMA

| Na. | Aina ya chanzo | Aina ya Huduma | Kiasi Tshs: |
|---|---|---|---|
| 1. | Choo cha Sokoni | Kuoga | 500 |
| | | Haja ndogo | 200 |
| | | Haja kubwa | 200 |
| 2. | Choo cha Stendi | Kuoga | 500 |
| | | Haja ndogo | 200 |
| | | Haja kubwa | 200 |
| 3. | Maeneo mengine | Kuoga | 500 |
| | | Haja ndogo | 200 |
| | | Haja kubwa | 200 |

SEHEMU YA TANO
USHURU WA VIWANDA VYA MATOFALI

USHURU WA VIWANDA VYA MATOFALI
Katika Maeneo yanayomilikiwa na Halmashauri –kwa mujibu wa mkataba

Katika maeneo yasiyomilikiwa na Halmashauri- Tshs 10,000/= kwa Mwezi

SEHEMU YA SITA
USHURU WA MAZAO YA BAHARI YANAYOUZWA KATIKA MNADA

| | | |
|---|---|---|
| Na. | 1. | Asilimia tatu (3%) ya bei ya mauzo |

SEHEMU YA SABA
USHURU WA KUSAFIRISHA SAMAKI NA MAZAO MENGINE YA BAHARI

| Na. | Aina ya Zao | Ushuru kwa kila kila moja shilingi |
|---|---|---|
| 1. | Samaki | 100/= |
| 2. | Dagaa | 100/= |
| 3. | Ngisi | 150/= |
| 4. | Kaa | 300/= |
| 5. | Kamba Miti | 250/= |
| 6. | Kamba Kochi hai | 1500/= |
| 7. | Kamba Kobe | 750/= |
| 10. | Mwami Mnene (Cottonii) | 30/= |
| 11. | Mwani Mwembaba (Spinosum) | 15/= |

*Tangazo la serikali Na. 1105(linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 12. | Vumbi la Dagaa | 100/= |
| 13. | Simbi | 15/= |

SEHEMU YA NANE
ADA YA MAOMBI YA KUJENGA VITUO VYA KUOSHEA MAGARI

| Na. | Eneo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Maeneo ya katikati ya Wilaya ya Kilwa | Tsh 50,000/= kwa mwaka |
| 2. | Nje ya maeneo ya katikati ya Wilaya ya Kilwa | Tsh 30,000/= kwa mwaka |
| 3. | Maeneo mengine | Tsh 10,000/=kwa mwaka |

SEHEMU YA TISA
ADA YA UKAGUZI WA AFYA KWA MAJENGO MAPYA YA BIASHARA

| Na. | Aina ya chanzo | | Kiasi Tsh. |
|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya kibali cha kuangamiza wadudu (fumigation) | Katikati ya Wilaya ya Kilwa | Tsh.20,000/= kwa kila Kibali |
| | | Pembezoni mwa Wilaya ya Kilwa | Tsh. 10,000/= kwa Kila Kibali |

SEHEMU YA KUMI
ADA YA KIBALI CHA KUFANYA SHUGHULI NYINGINEZO KATIKA MAENEO YA HALMASHAURI

| Na. | Huduma | Mhusika | Kiasi (Tsh) | Kipindi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kuweka matangazo ya picha (Display) | Taasisi | 300,000 | Mwaka |
| | | Watu binafsi | 200,000 | Kwa mwaka |
| 2. | Kufunga mtaa kwa ajili ya Shughuli mbalimbali isipokuwa shughuli za misiba, mikusanyiko ya kidini, michezo ya watoto isiyotozwa na mikusanyiko ya kisiasa | Barabarani na maeneo mbalimbali | Tsh,50,000/= | Kwa siku |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
ADA ZA MAOMBI YA ZABUNI MBALIMBALI ZA HALMASHAURI

| Na. | MAOMBI YA ZABUNI MBALIMBALI | Kiasi (Tsh) |
|---|---|---|
| 1. | Ukusanyaji wa mapato | 100,000/= |
| 2. | Ujenzi wa barabara | 100,000/= |
| 3. | Ukusanyaji na uondoshaji wa taka ngumu (CBD) | 100,000/= |
| 4. | Ukusanyaji na uondoshaji wa taka ngumu(pembezoni) | 50,000/= |
| 5. | Kupakua mashimo ya maji taka (vyoo) | 50,000/= |
| 6. | Kukarabati na kujenga maduka, Vioski na vizimba vya umma | 100,000/= |
| 7. | Kurekebisha mali za Halmashauri (magari na majengo) | 100,000/= |
| 8. | Ukaguzi na upimaji wa viwanja. | 100,000/= |
| 9. | Uendeshaji vyoo vya umma | 100,000/= |

*Tangazo la serikali Na. 1105(linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| 10. | Uendeshaji wa vioski vya Halmashauri | 100,000/= |
| 11. | Huduma ya ushauri elekezi (Consultancy services) | 100,000/= |
| 12. | Kukarabati na kujenga vibanda / Vizimba | 50,000/= |
| 13. | Ujenzi wa Majengo mbalimbali | 100,000/= |
| 14. | Huduma zisizohitaji ushauri wa kitaalamu (non-consultancy services) | 100,000/= |
| 15. | Ada ya maombi ya kazi ya ujenzi mtu binafsi (Local Fundi) kwa kutumiwa Force Account | 50,000/= |
| 16. | Ada ya Maombi ya Ujenzi kampuni Binafsi (ujenzi kutumia Force Account) | 100,000/= |
| 17. | Ada ya Maombi ya Ujenzi (Taasisi za umma) | 300,000/= |
| 18. | Ada za maombi ya zabuni katika Maeneo mengine ambayo hayajatajwa | 100,000/= |

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## ADA YA KUWEKA MAJENERETA

| Na. | Aina ya chanzo | Kiasi cha shilingi |
|---|---|---|
| 1 | Kuweka na Kutumia jenereta | 100,000/= kwa mwaka |

## SEHEMU YA KUMI NA TATU
## ADA YA UPIMAJI WA UBORA WA MAJI YA VISIMA, USAJILI WA JUMUIYA ZA WATUMIA MAJI, UKAGUZI, USIMAMIZI NA UFUATILIAJI WA JUMUIYA ZA WATUMIA MAJI NA MAOMBI YA KIBALI CHA KUTOA HUDUMA YA MAJI

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiasi cha shilingi |
|---|---|---|
| 1. | Upimaji wa Ubora wa Maji (Water Quality Analysis) | 150,000/= kwa mwaka |
| 2. | Usajili wa Jumuiya za Watumia Maji | 20,000/= kwa mwaka |
| 3. | Ukaguzi, Usimamizi na Ufuatiliaji wa Jumuiya za Watumia Maji | 50,000/= kwa mwaka |
| 4. | Maombi ya Kibali cha kutoa huduma ya maji | 50,000/= kwa mwaka |

## SEHEMU YA KUMI NA NNE
## ADA YA KIBALI CHA KUINGIZA KONTENA KWENYE ENEO LA HALMASHAURI

| Na. | Ukubwa Wa Kontena | Kiasi Kwa Kila Safari |
|---|---|---|
| 1 | Tani 3 hadi 10 | 50,000/= |
| 2 | Tani 11 hadi 20 | 100,000/= |
| 3 | Tani 21 hadi 30 | 150,000/= |
| 4 | Tani 30 na Kuendelea | 300,000/= |

## SEHEMU YA KUMI NA TANO
## ADA YA USAJILI NA USHURU WA KUEGESHA VYOMBO VYA UVUVI

| Na. | Ushuru wa kuegesha vyombo vya usafiri majini | Kiasi kwa mwezi |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa kuegesha vyombo vya usafiri majini | Tsh 30,000/= |
| 2 | Ushuru wa kuegesha vyombo vya kigeni | Asilimia 50% ya bei ya usajili wa chombo. |
| 3 | Ada ya usajili wa vyombo vya uvuvi | Tsh 20,000/= |

*Tangazo la serikali Na. 1105(linaendelea.)*

SEHEMU YA KUMI NA SITA
ADA ZA MATUMIZI YA FUKWE ZA BAHARI

| Na | ADA ZA MATUMIZI YA FUKWE ZA BAHARI | |
|---|---|---|
| 1. | Fukwe za bahari | Tshs 100,000/= kwa mwezi |

SEHEMU YA KUMI NA SABA
Ushuru wa Mgahawa Wazi (Open Air restaurant)

| Na. | Aina ya chanzo | Kiwango |
|---|---|---|
| | Mgahawa wazi *(Open air Restaurant)* | 5,000/= kwa siku |

SEHEMU YA KUMI NA NANE
Ada ya kibali cha kituo cha kulaza magari kwenye maeneo binafsi

| Na. | Aina ya Chanzo | Kiwango Kwa Mwaka |
|---|---|---|
| | Kibali cha kituo cha kulaza Magari katika Maeneo Binafsi | 200,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA TISA
ADA YA KUPATIWA MIHUTASARI YA HALMASHAURI

| Na. | Aina ya Chanzo | Tshs |
|---|---|---|
| 1 | Maombi ya Kupatiwa Muhtasari wa Halmashauri | 5,000/= kwa kila Muhtasari |

SEHEMU YA ISHIRINI
Ada ya Kibali cha kuendesha shughuli za gereji katika maeneo Binafsi

| Na. | Aina ya Chanzo | Tshs |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya gereji katika maeneo binafsi | 120,000/= kwa Mwaka |

*Tangazo la serikali Na. 1105(linaendelea.)*

______________

JEDWALI LA PILI

______________

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 18)*

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ………………………………………………………………………………nnakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ……………………………………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Kilwa, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya …… ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, niko tayari kulipa ada au ushuru ninaodaiwa kwa kiasi cha shilingi ....................... pamoja na faini ya kufifilisha kosa ya kiasi cha shilingi ...........................

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………….Mwezi………….Mwaka ......................................
Jina…………................................ Saini….........................................

MBELE YANGU :

Jina:…………………………………..……………………….....
Saini…………………………..…………………………..……
Wadhifa: …………………………………………………………
Tarehe……………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imegongwa kwenye Sheria ndgo hizo kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano mkuu wa baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya kilwauliofanyika tartehe 9/11/2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

HANAN M. BAFAGHI,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Kilwa*

MHE. ISSA B. MATEKA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Kilwa*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
29 Oktoba, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI*